



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

MKURUGENZI MKUU LATRA ATOA POLE KWA MKUU WA MKOA WA DODOMA

Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, CPA Habibu Suluo, ametoa salamu za pole kwa Mhe. Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, kufuatia vifo vya watu 12 na majeruhi 63 vilivyotokana na ajali iliyotokea Alhamisi, tarehe 9 Februari, 2023 saa 07:05 usiku eneo la Silwa mpakani mwa mkoa wa Morogoro na Dodoma, tarafa ya Kibaigwa Wilayani Kongwa mkoani Dodoma.

Ajali hiyo ilihusisha gari la mizigo aina ya Scania lenye namba ya usajili T128 DUB likivuta tela lenye namba ya usajili T677 DVX na basi la abiria kampuni ya Frester lenye namba ya usajili T415 DPP iliyokuwa inatoka Bukoba kuelekea Dar es Salaam.

Katika salamu zake, CPA Suluo ametoa pia pole kwa familia, ndugu, jamaa na wafiwa wote; vilevile amewapa pole majeruhi na kuwaombea uponaji wa haraka.

Mfumo wa LATRA wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS) unaonesha kuwa basi hilo la abiria lilitoka Stendi Kuu ya Mabasi Bukoba tarehe 8 Februari, 2023 saa 12:01 asubuhi, na lilipata ajali hiyo lilipofika Silwa. LATRA kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani wameanza uchunguzi wa kina ili kubaini chanzo cha ajali hiyo kwa lengo la kuchukua hatua stahiki za kuzuia ajali za aina hii.

Aidha, LATRA inawakumbusha madereva wote wa vyombo vya usafiri kibiashara kufika ofisi za LATRA katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ili kusajiliwa na hatimaye kuthibitishwa kwa mujibu wa kifungu cha 5(1)(e) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 na Kanuni za Usajili wa Wahudumu na Uthibitishaji wa Madereva za mwaka 2020.

Imetolewa na:

Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano – LATRA
09 Februari, 2023